*SWAHILI FORUM 21 (2014): 26-39*

# SANAA KWA MAENDELEO TANZANIA: KATI YA KUJIWEZA NA KUWEZWA

VICENSIA SHULE

Theatre for Development (TfD) is a process whereby the community uses theatre, especially African traditional theatre forms, to address their development issues. In Tanzania, TfD came as a result of many factors; poor communication approaches used by the state in addressing development in the late 1970s, the economic crisis of the 1970s, the implementation of IMF and World Bank pressure to adopt Structural Adjustment Programs (SAPs) among others. Liberal policies imposed mostly from Euro-America proposed non-governmental organizations (NGOs) to replace the state in addressing development, as they were perceived to be more democratic and less authoritative. Most of the supported activities of NGOs became those linked to development or that are in the position to bring about development in the fields of health, sanitation, education, gender, and democracy. Therefore, even theatre that was supported by donors was linked to or addressed 'development'. In most cases, funding institutions have their own objectives, missions, and goals to fulfil. This paper tries to question the role of TfD in present Tanzania. It argues that, since most of the TfD projects have been funded by foreign donors and communities have no economic control of their own development concerns, it is clear that TfD is playing a double deal, community empowerment on the one hand and disempowerment on the other.

## Utangulizi

Sanaa kwa Maendeleo (SkM) ni dhana ya kutumia sanaa hasa za maonesho ili kumwezesha mwanajamii kujiletea maendeleo yake mwenyewe. Mbinu ya Sanaa kwa Maendeleo au SkM kwa kiasi kikubwa imejikita katika kuamini kuwa ikiwa jamii fulani ina matatizo ya kimaendeleo, ni wanajamii wenyewe ndio wenye uwezo wa kuyajadili na kuyapatia ufumbuzi. Ingawa dhana hii siyo ngeni masikioni mwa wanajamii na wanaharakati wa maendeleo, imekuwa ikitumika kama kielelezo kuonesha mchango wa sanaa katika kuleta maendeleo kwa Mtanzania, Mwafrika na sehemu nyingine duniani ambako imekuwa ikitumika. Kwa lugha ya Kiingereza dhana hii imekuwa ikitambulika zaidi kama *Theatre for Development* au *TfD*. Hii inamaanisha kuwa neno la 'sanaa' linatumika kama mbadala wa neno la 'tamthilia'. Hii haimaanishi kuwa katika jamii ya wazungumzaji Kiswahili hakuna tamthilia, bali ni kutokana na ukweli kuwa neno la 'sanaa' limekuwa likitumika kuwasilisha dhana ya sanaa yoyote iwe ya ufundi au maonesho.

Lengo la makala hii ni kuangalia undumilakuwili wa Sanaa kwa Maendeleo (SkM) katika miradi inayofadhiliwa toka nje hasa katika ile inayojihusisha na maendeleo katika jamii ya Tanzania ya leo. Dhana ya undumilakuwili katika makala haya inatumika kuonesha pande mbili zinazokinzana za SkM – kati ya kujiweza (*empowerment*) na kuwezwa (*disempowerment*). Dhana hizi mbili zimekopwa toka kwenye hotuba ya Profesa Ngũgĩ wa Thiong'o aliyoitoa katika mhadhara wa wazi uliofanyika ndani ya Ukumbi wa Nkrumah, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tarehe 22 Novemba 2013. Hotuba hiyo ilijulikana kama *Wasomi, Lugha za Ulaya na za Afrika: Kati ya Kujiweza na*

*Kuwezwa* (Ngũgĩ wa Thiong'o 2013). Ingawa Ngũgĩ alizitumia dhana hizi kuelezea mkanganyiko unaowakumba wasomi wa Kiafrika katika kuchagua lugha ya/za kuwasiliana, zinaweza pia kuelezea mkanganyiko na undumilakuwili wa SkM.

Sanaa ni chombo kinachoweza kuionesha jamii kama ilivyo (*simulacrum*). Marvin Carlson (2001: 2) anasisitiza hilo kwa kuonesha umuhimu wa sanaa za maonesho katika kuweka sawa utamaduni na historia ya jamii. Kutokana na nadharia hiyo hiyo, SkM inaonekana kuwa 'zao' la jamii kulingana na uwezo wake wa kutumia fani mbalimbali za sanaa za maonesho zilizopo katika jamii husika kama vile ngoma, hadithi, maigizo, nyimbo, mashairi, miviga na nyinginezo. Fani hizi ndio msingi wa sanaa za maonesho katika jamii nyingi za Kiafrika.

Makala hii inawasilisha wazo kuu kuwa ingawa SkM inafanya kazi kubwa ya kuiwezesha jamii kujitambua, kujitafakari na kuchukua hatua dhidi ya matatizo iliyonayo, SkM hiyo hiyo inafanya kazi ya kuizuga jamii husika isiweze kutambua asili ya matatizo na namna sahihi ya kutatua matatizo hayo. Makala haya yamegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza inasimulia historia ya SkM nchini Tanzania. Sehemu ya pili inaangalia namna mbalimbali ambavyo SkM imekuwa ikitumika katika kuifanya jamii ijiweze. Mwisho ni uchambauzi wa undumilakuwili wa SkM katika jamii hususani dhana ya kuwezwa.

## Historia ya Sanaa kwa Maendeleo nchini Tanzania

Kabla ya kuanza kutumika nchini Tanzania, mbinu ya Sanaa kwa Maendeleo (SkM) imetumika maeneo mengi ulimwenguni. Mlama (1991: 23) anaonesha jinsi ambavyo tawala za China na Kuba zilivyotumia sanaa kama njia madhubuti ya kujenga ukomunisti katika miaka ya 1950. Harakati za sanaa zilichangia kwa sehemu kubwa katika kuangusha tawala za Marcos nchini Ufilipino na ile ya Samosa nchini Nicaragua katika miaka ya 1970 (Epskamp 2006: 1). Katika bara la Afrika, mfano wa SkM iliyoleta mafanikio ni ile ya Kamiriithu nchini Kenya iliyoongozwa na Ngũgĩ wa Thiong'o. SkM hiyo ndiyo iliyozaa mchezo wa *Nitaolewa Nikipenda* mwaka 1977 ambao ulisababisha Ngũgĩ kupata misukosuko ya kisiasa chini ya utawala wa rais Daniel Arap Moi (Odhiambo 2008: 83). Mifano hii inaonesha nguvu ya SkM katika jamii iwapo itatumika kama silaha ya kujiweza.

SkM ilianza kutumika Tanzania mwishoni mwa miaka ya 1970 na mwanzoni mwa miaka ya 1980 (Mlama 1991: 67). Ingawa wakati wa ukoloni kulikuwa na matumizi ya sanaa kama vile filamu katika 'kumstaarabisha' Mwafrika, muktadha wa matumizi ya sanaa wakati wa ukoloni unatofautishwa na matumizi ya SkM inayojadiliwa katika makala hii. Sanaa iliyokuwa inatumika wakati wa mkoloni haikulenga kumfanya Mwafrika ajitambue ili ajikomboe, bali kumlazimisha kujiona mnyonge, mtu mwenye tamaduni za kishenzi ambaye anahitaji sanaa imsaidie 'kustaarabika' (Lihamba 2004: 236).

Mwishoni mwa miaka ya 1970 ulikuwa ni wakati ambao Tanzania ilikuwa inakabiliwa na kipindi kigumu kiuchumi. Mambo mengi – ya ndani na nje – yalichangia katika kuteteresha uchumi wa Tanzania. Kwanza, Watanzania walikuwa ndio wametoka katika kutekeleza awamu mbalimbali za Azimio la Arusha la mwaka 1967. Utekelezaji wa Azimio la Arusha uliambatana na utaifishaji wa vitu mbalimbali – majengo, biashara na kampuni ambazo zilimilikiwa na 'mabepari'.

Hii ilikuwa ni kutekeleza lengo kuu la Azimio la Arusha kwamba njia kuu za uchumi ni lazima zimilikiwe na umma. Azimio la Arusha pia lilielekeza wananchi kukaa katika Vijiji vya Ujamaa (Operesheni Vijiji) ili waweze kupatiwa huduma muhimu za kijamii. Harakati hizi za kutekeleza Azimio la Arusha zilipingwa na baadhi ya watu, na wengine wakipongeza (Askew 2002: 237; Shivji 2009: 44).

Kulifuata Vita vya Kagera mwaka 1978/1979. Vita hivi vililenga kupambana na Iddi Amin, rais aliyejitwalia madaraka nchini Uganda kwa mapinduzi ya kijeshi. Iddi Amin alitangaza kutwaa sehemu ya Tanzania akiamini ni sehemu ya Uganda. Kulikuwa vilevile na kipindi kirefu cha ukame uliosababisha njaa kali katika miaka ya mwanzo ya 1980 (Fosu 2008: 145; Lange 2002: 64). Katika ngazi ya kimataifa, kulikuwa na mfumuko wa bei ya mafuta ulimwenguni. Zaidi, sera za Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia zililazimishwa kutumika kama njia pekee ya kuunusuru uchumi wa nchi zilizokuwa zinayumba (Chachage & Chachage 2004: 44).

Miaka kati ya 1970 hadi mwanzoni mwa 1990 ni wakati ambao 'chama kilikuwa kimeshika hatamu'. Ulikuwa ni wa wakati wa chama kimoja cha siasa kuongoza mamlaka ya dola na tunaweza kukiita chama-dola. Maana yake ni kuwa utawala wa serikali na ule wa chama cha siasa haukuwa na tofauti. Mfano, mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mwalimu Julius Nyerere ndiye aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na viongozi wengine kama Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Jaji Mkuu na wengineo walikuwa wanashika nyadhifa ndani ya chama. Katika ngazi ya wilaya na mkoa wakuu wake ndio waliokuwa wenyeviti wa CCM katika maeneo yao. Kutokana na hali ngumu ya uchumi na viongozi kuhodhi madaraka makubwa, Watanzania wangelipenda kuhoji uhalali na utendaji usioridhisha wa serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM). Hata hivyo, fursa za kuhoji uhalali wa sera na viongozi walioshindwa kuleta maendeleo zilikuwa adimu kutokana na ukiritimba uliokuwa ukiminya uhuru wa kusema. Kulihitajika mbadala wa kuwapa Watanzania katika ngazi ya jamii fursa ya kupitia upya matatizo yao, kutafakari na kuhoji bila kukumbana na 'mkono wa dola'. Sanaa ilikuwa ni moja ya njia chache za kuwezesha majadiliano hayo.

Wataalamu wa sanaa kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakiongozwa na Amandina Lihamba, Penina Mlama na Eberhardt Chambulikazi, kama waasisi wa SkM nchini Tanzania, walijaribu kutumia sanaa kama njia ya kutafuta suluhisho kwa changamoto zilizokuwa zinaikabili jamii. Wazo la kuanzisha harakati za SkM nchini Tanzania lilitokana na ushiriki wa Lihamba na

Chambulikazi katika warsha ya SkM iliyofanyika nchini Zambia mwaka 1978 (Kerr 1995: 154). Warsha ya Zambia ilikuwa ni mwendelezo wa warsha ya awali iliyofanyika nchini Botswana mwaka 1978 ikijadili namna ya kutumia sanaa hususan za maonesho katika kuchangia maendeleo ya bara la Afrika kwa wakati huo. Lengo hasa la SkM nchini Tanzania lilikuwa ni kuiwezesha sanaa kutumika katika kuamsha ari na kuwawezesha wanajamii kupata fursa ya kujadili na kuhoji mambo mbalimbali yanayokwamisha maendeleo yao kupitia maonesho. SkM ililenga kuhakikisha kuwa wanajamii wanashiriki katika shuguli za kujiletea maendeleo kwa manufaa yao wenyewe. Ndio maana hadi leo SkM inafahamika kama sanaa ya watu, kwa ajili ya watu toka kwa watu, kwenda kwa watu (*popular/people's theatre*).

## Matumizi ya Sanaa kwa Maendeleo

SkM ya Afrika na hususan ile ya Tanzania imejijenga katika misingi ya matumizi ya sanaa kama zana ya ukombozi wa wanyonge – *Pedagogy of the Oppressed* – iliyojengwa na Augusto Boal. Boal (2000: xxi) anaamini sanaa ni zao la jamii. Hivyo basi sanaa hiyo ni lazima imilikiwe na ifaidishe jamii hiyo. Kwa kuwa chini ya umiliki wa jamii, sanaa hiyo lazima isaidie ujenzi wa maendeleo ya wanyonge wa jamii husika. Maana yake ni kuwa wanyonge wa jamii fulani hawawezi kukombolewa na sanaa ya kigeni ambayo sio zao lake. Ni vyema kwa jamii husika kuwa na maamuzi ya mwisho kwenye utumiaji wa sanaa ili iwe silaha ya kujiweza.

Historia ya matumizi ya sanaa kwa ajili ya kusaidia jamii mbalimbali barani Afrika ilianza mara tu baada ya nchi nyingi kupata uhuru. Kwa Tanzania, wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia Idara ya Sanaa (ikiitwa Art, Music and Theatre) walianza kwa kupitia sanaa za jamii mbalimbali kabla ya ukoloni. Hii ilifanyika ili kuona namna gani sanaa zinaweza kutumika kama njia ya kuelezea hali halisi iliyokuwepo (Lihamba 1985: 91). Kulikuwa na mifumo mbalimbali iliyojadiliwa, ila mfumo uliopendekezwa ni ule wa 'kupeleka' sanaa kwa jamii. Mfumo huu ulitumia walimu na wanafunzi wa Chuo Kikuu kuandaa onesho na kusafiri sehemu mbalimbali kulionesha. Mfumo huu wa kupeleka sanaa kwa jamii ulikumbwa na mapungufu kadhaa. Moja kubwa ni kuona kama vile jamii haina sanaa bora hivyo kwa kupeleka onesho lililoandikwa na 'wataalamu' wa sanaa ni njia mojawapo ya kuwafunza wanajamii jinsi ya kuandaa sanaa bora. Kutokana na mwitikio hafifu toka kwa wanajamii hasa pale wanajamii waliposhindwa kuelewa lengo la onesho la wanazuoni, ilibidi kubadilisha mfumo. Wanazuoni waliona badala ya kuandaa onesho na kulipeleka ni bora kwenda kukaa katika jamii fulani, kujifunza sanaa na mazingira yao, kisha kurudi na kuandaa onesho. Onesho lilipokamilika walilirudisha kwa wanajamii ili kuanzisha au kuchochea mijadala. Pamoja na jitihada hizo, bado maonesho ya aina hiyo hayakuweza kuifanya jamii ijione sehemu ya onesho na hata ushiriki wa wanajamii katika mijadala ulibaki kuwa wa kufikirika, usiojikita katika kuchambua jamii husika ili iweze kuondoa kero za maendeleo (Bakari & Materego 2008: 18).

Hivyo, dhana ya Sanaa kwa Maendeleo (SkM) ilipojitokeza ilisaidia 'kutibu' changamoto na mapungufu yaliyosababishwa na mifumo ya kupeleka sanaa kwa jamii na ule wa kuiandalia jamii sanaa. Kama ilivyogusiwa hapo awali, SkM inatumia wanajamii wenyewe toka mwanzo hadi mwisho wa uandaaji wa maonesho. Hata mijadala wakati na baada ya onesho huongozwa na wanajamii wenyewe. SkM hufanyika kwa kupitia hatua mbalimbali. Kwa mujibu wa Juma Bakari and Ghonche Materego (2008: 41-66) zipo hatua tisa. Kwanza ni kuchagua jamii ambayo SkM itafanyika. Pili ni kuyazoea mazingira, tatu ni kufanya utafiti wa matatizo. Nne, ni kucchambua matatizo yaliyojitokeza. Hatua ya tano ni uundaji sanaa na sita ni maonesho. Baada ya hapo majadiliano hufuata, kisha tathmini hufanyika na mwisho kabisa ni ufuatiliaji. Hatua ya pili hadi ya nane huweza kufanyika katika kipindi cha siku saba au zaidi kulingana na mpangilio mzima wa SkM. Tathmini inayofanyika hapa ni ya awali, mara tu baada majadiliano. Ufuatiliaji hufanyika kulingana na maazimio yaliyopitishwa na mara nyingi hufanyika baada ya miezi sita, mwaka au miaka. Wakati mwingine tathmini haifanyiki kabisa na nitafafanua sababu mbalimbali zinazosababisha hali hiyo.

Mafanikio ya SkM kwa kipindi cha miaka ya 1980 hadi mwishoni mwa 1990 yanawezesha kusema kuwa ni kati ya mbinu zinazoweza kuwapa wanajamii fursa za kipekee za kuyachambua maisha yao kulingana na mazingira wanayoishi, huku wakiburudika. Pia ni mbinu ya kimapinduzi iliyoweza kuwanyang'anya 'hatamu' viongozi wazembe pale wanajamii wanapopata fursa ya kuchangia hoja na kufanya maazimio yao. Kwa kuonesha manufaa na mafanikio ya SkM, wataalamu wengine wametoa wito wa matumizi ya mbinu hii ili kuharakisha maendeleo (Bakari & Materego 2008; Etherton 2004; Eyoh 1984). Koch (2008: 113) anaonesha wazi kuwa miradi mingi ya awali iliweza kuleta mafanikio makubwa kutokana na uhuru uliokuwepo toka kwa wafadhili. Wafadhili hawakuchagua jamii na malengo ya kufanyika kwa SkM bali waliwaachia wanajamii wakisaidiwa na waraghibishi.

Mlama (1991) amechambua baadhi ya warsha za SkM zilizoleta mafanikio makubwa. Mfano ni zile za Malya-Mwanza (1982-83), Msoga-Pwani (1983), na Mkambalani-Morogoro (1986). Katika SkM iliyofanyika Malya, wananchi waliweza kutengeneza onesho walililoliita *Walanguzi* (Mlama 1991:133). Onesho hili lilifichua jinsi viongozi mbalimbali wanavyoshiriki katika vitendo vya kuhujumu uchumi, hivyo kuwa njia ya kuvipatia vyombo vya dola taarifa kuhusu mambo yanayotokea katika ngazi ya jamii ambayo yanapingana na malengo ya serikali. Katika andiko jingine nilieleza mafanikio na changamoto ya warsha nyingine zilizofanyika kuanzia mwaka 2000 kama vile ile ya Mlonganzila-Pwani (2000), Temeke-Dar es Salaam (2004) na Pangani-Tanga (2009). Mafanikio yaliyojitokeza katika warsha ya Mlonganzila ni kwa wanawake kuweza kujadili na kuwasilisha mawazo yao mbele ya jamii. Jambo ambalo halikuwahi kufanyika kutokana na mfumo wa uongozi uliokuwepo ambao haukuwa unawapa wanawake fursa ya kuelezea matatizo yao (see Shule 2010: 144-245).

Kumbukumbu zinazoelezea mafanikio na changamoto za warsha za SkM ziko katika ofisi na maktaba za mashirika fadhili kama OXFAM, United Nations Children's Fund (UNICEF), Dutch Organization for Development (HIVOS), Swedish International Development Coorporation Agency (SIDA), United States Agency for International Development (USAID), Deutsche Gesellschaft für Technische Zusammenarbeit (GTZ). Kwenye asasi za umma kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) na asasi zisizo za kiserikali kama Uzima kwa Sanaa (UZIKWASA), Population Service International (PSI), Tanzania Gender Networking Programme (TGNP), Tanzania Media Women's Association (TAMWA), Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA) na nyinginezo.

Pamoja na kuiwezesha jamii, SkM hutumika kama mbinu ya utafiti katika tafiti na miradi mbalimbali (Koch 2008; Epskamp 2006; Materego 2002). Mafanikio haya ya SkM yameweza kutoa zao jipya – *Tuseme*[1]. *Tuseme* ilianza kama mradi nchini Tanzania katika Idara ya Sanaa na Sanaa za Maonesho ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1996 ikisimamiwa na Amandina Lihamba na Penina Mlama. *Tuseme* kwa kiasi kikubwa imeleta mafanikio makubwa kwa jamii za Tanzania na Afrika kwa ujumla kwa kuwezesha watoto wa kike kujiamini, kujadili kwa uwazi kero zao na pia kuweza kufaulu vizuri (Mlama 2005; Ziegler 2009; Lihamba 2007). Mafanikio hayo ya *Tuseme* yameiwezesha kuenea katika nchi zaidi ya 17 barani Afrika (Mlama 2005).

## Undumilakuwili wa Sanaa kwa Maendeleo

Hivi sasa Sanaa kwa Maendeleo (SkM) imefanikiwa kuwa sehemu ya mikakati na miradi mbalimbali kwa sifa yake ya kuwa mbinu shirikishi. Pia SkM imekuwa ikitumika kama njia mojawapo ya kufanya utafiti ili kupata taarifa zitakazosaidia kuboresha maisha ya wanajamii. Waraghibishi au wawezeshaji kutoka nje ya jamii wakishirikiana na wanajamii hupitia hatua zote za SkM kwa lengo la kuwajengea uwezo waraghibishi wa ndani ili waweze kuendeleza mchakato pale wawezeshaji toka nje ya jamii watakapoondoka. Hivyo wanajamii wenyewe ndio wanaotakiwa kuchukua jukumu la kuendesha mijadala wakati au baada ya maonesho ili kuonesha maana halisi ya SkM kuwa sanaa ya jamii kwa ajili ya wanajamii inayofanywa na wanajamii wenyewe.

Tangu ilipoanza miaka ya 1980, mambo mengi yamebadilika kisiasa, kiuchumi, kijamii na hata kiutamaduni. Ilitegemewa kuwa kwa kuwa ni mbinu shirikishi yenye kulenga katika kutoa fursa za kujadili mambo mbalimbali yanayohusu maendeleo iwe imejikita katika jamii na kuwa mbinu endelevu. Lakini kwa sehemu kubwa, haijawa hivyo. Zaidi ya miaka 30 imepita toka SkM imeanza kutumika, bado imejikita katika kutumia waraghibishi toka nje ya jamii husika, Ghonche Materego

[1] *Tuseme* ikiwa na maana ya 'tusikae kimya, tuzungumze', ni mbinu ya kutumia SkM katika shule za msingi na sekondari kuwapatia watoto, hasa wa kike, fursa ya kutafiti, kuibua, kuzungumza na kujadili changamoto zinazowakabili katika elimu na hivyo kufifisha ufaulu wao na kuzitafutia ufumbuzi.

(2002: 24-25) ameonesha wazi kuwa mara nyingi SkM huishia pale waraghibishi kutoka nje wanapoondoka. Hii inatokana na ukweli kuwa ingawa SkM ni mali ya jamii, inayofanywa na wana-jamii, toka katika jamii, kwa ajili ya jamii, umiliki wake uko mikononi mwa wanaotoa wazo na fedha za kuendesha mchakato huo katika jamii fulani. Kwa muda mrefu SkM imekuwa ikipata ufadhili kutoka kwenye mashirika ya kimataifa. Hapa tunazungumzia 'ufadhili mkubwa' wa fedha za kuweza kuleta wazo la kufanya SkM katika jamii fulani. Iwapo hakuna ufadhili ni nadra kwa SkM kufanyika au mradi hufa baada ya ufadhili kwisha (Shule 2011: 201). Kuna msemo usemao, 'anayemlipa mpiga zumari, ndiye anayechagua wimbo'. Maana yake ni kuwa pamoja na nia njema ya wafadhili katika kufanikisha SkM, bado kuna namna fulani ambayo ufadhili unachangua nini kifanyike na nini kisifanyike au kifanyike vipi.

Julius Nyerere (1968: 25) alionya mapema kuwa, mtu huwezi kuwa unategemea ufadhili na bado ukabaki huru. Ufadhili, zawadi na mikopo toka nje ni vitu vinavyohatarisha uhuru wa Watanzania. Nyerere pia ameonesha kuwa hakuna tofauti yoyote kati ya uhuru na utumwa pale mtu anapotegemea ufadhili. Anasisitiza kuwa, ikiwa ni kupata maendeleo, wanajamii wenyewe ndio wanaotegemewa kuchukua jukumu la maendeleo na siyo kutegemea wafadhili. Ingawa kuna maswali mengi katika dhima na dhana ya ufadhili, hali hii haiondoi ukweli kuwa wafadhili wana mchango katika maendeleo ya Watanzania. Suala la msingi hapa ni kwa namna gani michango hii ya wafadhili inazindua ari ya serikali katika kuwapatia maendeleo wananchi wake ambalo ndilo jukumu kuu la serikali yoyote ile iliyopo madarakani. Tangu kuanza kutumika kwa SkM miaka ya 1980 hadi sasa mambo mengi yamebadilika nchini Tanzania. Wakati wa siasa ya ujamaa, iliaminika kuwa maendeleo yanaletwa na watu na 'pesa haikuwa msingi wa maendeleo'. Lakini katika muktadha wa sasa wa ubepari na siasa za uliberali mamboleo, pesa inaonekana kama ndio msingi wa maendeleo. Hivyo SkM inalazimika au kulazimishwa na mfumo kubadilika ili 'kuendana' na muktadha. Hali hii inaweza kusababisha SkM kupoteza umiliki wa wananchi ambao ilikuwa nao wakati ilipobuniwa. Na kwa kuwa maendeleo ya sasa yanatokana na pesa na si watu, ni wazi SkM nayo inaweza ikajikuta mikononi mwa wachache wenye pesa wakiitumia watakavyo na si lazima katika lengo la kumwezesha mwananchi ajitambue na kupambania maendeleo yake.

Hivi sasa kumeibuka matumizi mapya ya SkM. Miradi mingi inayolenga maendeleo imelazi-mishwa kutumia sera za utamaduni na mbinu shirikishi (Diagne & Ossebi 1996: 28-29; Wallace, Bornstein, & Chapman 2007: 41). Ndagala (2007: 3) anatuambia kuwa hata Benki ya Dunia sasa nayo imetambua umuhimu wa utamaduni na maendeleo. Kwa kuwa SkM ni moja kati ya mbinu shirikishi, imekuwa ikitumika katika miradi inayofadhiliwa na mashirika hayo. Changamoto iliyopo ni kuwa mfumo wa dunia umetawaliwa na ubepari, ubeberu na uliberali mamboleo hivyo siyo rahisi kwa mfadhili kuja kumsaidia Mtanzania kujikwamua bila kuwa na malengo. Amartya Sen (2000) amesema wazi kuwa, ulimwengu wa mabenki na ule wa utamaduni hauna mambo mengi yanayolandana. Hivyo si rahisi kuweka dhana hizi mbili (ulimbikizaji wa mtaji na

utamaduni) kwenye kapu moja. Hivyo, ni wazi kuwa ufadhili wa SkM ni lazima uendane na matakwa ya mtoa fedha, la sivyo si rahisi kwa 'wenye' fedha kuwekeza kwenye SkM. Inasemekana kuwa sasa hivi wafadhili nao wanakuja kwa msukumo wa 'kibinaadamu' kumletea Mwafrika maendeleo. Msukumo huu hauna tofauti na ule ambao uliwaleta wamisionari wakati wa ukoloni kuja kukomesha biashara ya utumwa na kumstaarabisha Mwafrika. Maendeleo haya kupitia mipango ya maendeleo ya uchumi (Structural Adjustment Programs - SAPs) ya Mfuko wa Fedha wa Dunia (IMF) na Benki ya Dunia na mengine yenye sura hiyo, yanalazimisha watu kuamini kuwa kupitia utandawazi 'dunia sasa ni kijiji'. Shivji (2007: 1) anaonya kutobweteka katika mapambano dhidi ya mifumo gandamizi kwani uliberali mamboleo unawakilisha ushari wa kurudi kwa ubeberu katika mfumo wa utandawazi. Shivji anaendelea kusisitiza kuwa, ni lazima kutia shaka maendeleo yanayoshinikizwa kupitia utandawazi. Ingawa maendeleo yanayolengwa na SkM ni yale ya kubadilisha fikra za watu ili waweze wenyewe kushiriki shughuli za kuleta manufaa kwa jamii, kuna haja ya kuchambua kwa kina lengo la SkM inayosukumwa na sera za kiliberali mamboleo. Kwani iwapo SkM itafungamana na uliberali mamboleo na kuwa na ajenda inayofanana, huenda jamii na wanajamii sio kipaumbele au wadau wakuu.

Tangu kuanza kutumika kwa mbinu ya Sanaa kwa Maendeleo (SkM), kumekuwa na mabadiliko mengi ya kiutendaji na kiitikadi. Dhana ya maendeleo ya watu toka kwa watu kwa manufaa ya watu, imemezwa na sera za wafadhili. Miradi inayoandikwa ni lazima iende sambamba na sera za wafadhili hata kama hazimsaidii Mtanzania (Shule 2010: 243). Jane Plastow (2009: 17) anajaribu kuhoji umuhimu wa SkM katika Afrika ya leo, kama kweli ni mbinu ya kuwawezesha wanajamii au ni zana ya kuwagandamiza. Pia anahoji iwapo waraghibishi wa SkM wako makini katika kutumia mbinu hii wanapoiandika katika miradi yao au suala la msingi ni kuangalia fedha za wafadhili na jinsi ya kuzipata. Kwa ujumla Plastow (2009: 17) anaona SkM kama biashara, utaratibu wa kumyanganya uwezo (kuwezwa) mwanajamii na zana jadidi ya kumgandamiza. Suala la kuhakiki iwapo mambo yanayofanyika katika jamii ni ya manufaa au la, ni jukumu la serikali na viongozi. Hivyo basi kuna haja ya kuishauri serikali kuwa macho kuangalia manufaa ya miradi inayofadhiliwa.

Materego (2002: 24), Samba (2005: 24) na Nyoni (2008: 170-172) kwa upande wao wanaona mchakato wa SkM umejikita katika kuiangalia jamii kutoka juu na mara nyingi unashindwa kuiwezesha jamii katika ngazi ya chini kabisa. SkM inayofanyika chini ya ufadhili wa mashirika ya kigeni haiwajali wanajamii, bali inazingatia kuwa ujumbe uliotolewa na mfadhili umefika. Wakati mwingine hata kama ujumbe huo hauendani na mtazamo au hautatui matatizo ya jamii husika, 'utapachikwa' katika SkM na kuwasilishwa. Wakati wa kuandika ripoti ni wazi kuwa wenye mradi wataonesha kuwa maoni na mawazo yaliyotolewa ni ya wanajamii kwani wametumia mbinu shirikishi kuyapata. Wanazuoni hawa wa SkM wanashauri uwepo wa mapitio ya matumizi ya SkM ili iweze kufanya kazi yake iliyobuniwa ya kumkomboa mwanajamii kifikra.

Kwa upande wa sanaa, SkM imegeuka kuwa njia mojawapo ya kuififisha na kuinyang'anya jamii amali yake. Kama ambavyo Boal (2000) anaonesha, sanaa ni zao la jamii kwa matumizi na manufaa ya jamii hususan wanyonge. Sanaa imekuwa ikitumika kuburudisha, kuelimisha, kutunza kumbukumbu, kukosoa na hata kuleta ukombozi. Kwa kuendelea kutumia SkM kwa lengo la kufikisha ujumbe tu ni dhahiri mizania ya dhima nyingine za sanaa kama burudani na umbuji zimemezwa (Epskamp 2006: 62; Shule 2010: 166-167). Kumekuwa na wasiwasi kuwa kuendelea kutumia sanaa zisizosanifishwa katika SkM ni kushusha hadhi ya sanaa za maonesho. Kiujumla Kerr (1995: 155) anakiri kuwa iwapo SkM inafuata mfumo wa sanaa za Kiafrika, ni kuzidhalilisha kwani hata sanaa za maonesho zilizokuwepo kabla ya ukoloni zilikuwa zenye kuweka mizania katika ubora na umbuji na hazikuwa sanaa za hovyo hovyo.

Vilevile, SkM imekuwa kati ya mbinu zinazonyonya amali ya jamii kwa manufaa yake. Kwa mfano, wakati wa kutumia SkM, sanaa na wasanii wanaotumika huwa haviangaliwi. Hakuna uwekezaji unofanyika katika sanaa zaidi ya SkM kujikita na kujipambanua kama mbinu ya uraghibishi (Shule 2010: 168; Kerr 1995: 62). Kwa wasanii, kufanya kazi katika miradi ya maendeleo, mara nyingi huwapatia wasanii kipato kizuri wakati wa mradi. Mradi unapokwisha, na malipo yanakuwa yamekwisha. Ubunifu wa wasanii unamezwa na mifumo ya miradi na hata uhuru wao unafungwa kwani wasanii hawawezi kufanya jambo lolote nje ya andiko la mradi au mtazamo wa wafadhili. Ikiwa lengo la SkM ni kufikisha ujumbe tu na si umbuji wa sanaa yenyewe, au lengo ni mawasiliano na si mchakato wa kuwapatia wasanii stadi za sanaa yenyewe, matokeo yake ni kuwafanya wasanii kuwa tegemezi mradi unapokwisha kwani wengi wao wanapata shida ya kuuza sanaa zao ambazo wamekuwa wakizionesha 'bure' kwa jamii chini ya ufadhili wa miradi.

Mwanzoni mwa makala haya nilizungumzia suala la ufuatiliaji na niligusia kuwa wakati mwingine haufanyiki. Ukweli ni kuwa iwapo mfadhili au mtafiti atakuwa amepata taarifa alizokuwa anatafuta hatakuwa na haja ya kurudi kufanya ufuatiliaji (Epskamp 2006: 62; Shule 2010: 166). Vilevile iwapo mradi utatenga fungu kwa ajili ya kuwawezesha waraghibishi au watafiti kurudi katika jamii ili kufanya ufuatiliaji na mfadhili akaridhia, basi hilo litafanyika. Lakini kama hakutakuwa na uwezeshwaji wa kufanya ufuatiliaji au mradi utakuwa umefika ukingoni, siyo rahisi kwa mtu yeyote kujitolea kurudi kwenye jamii kufanya ufuatiliaji. Hili halikuwa lengo kuu wakati SkM ilipoanza kutumika miaka ya 1980. Lengo ni kufanya wanajamii 'wajiweze' na waweze kuendeleza mbinu hii ya SkM pale waraghibishi na wafadhili toka nje wanapoondoka. Changamoto iliyopo kwa sasa ni kuwa SkM mara nyingi haianzishwi na wanajamii wenyewe, bali kundi la waraghibishi na watafiti wanaotaka kuingilia jamii na kutaka kuwaelekeza jinsi ya kuyatambua matatizo yao ambayo mfadhili angependa kuyashughulikia. Hivyo ni rahisi kutumika vibaya kwa ajili ya kumnufaisha mfadhili, mraghibishi au mtafiti.

Kama anavyobainisha Plastow (2009: 1) SkM imekuwa kama biashara. Biashara nzuri huangalia faida, na kama faida imeshapatikana basi kuna njia mbili; kuboresha biashara (kuandika miradi mingi zaidi) au kutumia mtaji kuanzisha biashara mpya. Tabia hii ndio hasa inayoongoza wafadhili, waraghibishi na watafiti kwenda kwenye jamii. Sababu nyingine ni kuwa SkM sasa imepachikwa tu katika jamii, hivyo wanajamii hawaoni sababu ya kuendeleza kitu kisichokuwa chao. Pia mara nyingi katika hatua ya kuchambua matatizo wanajamii wamekuwa wakijitoa na kuwanyooshea viongozi wao vidole kama vikwazo vya maendeleo. Dhana hii ni hatari kwani SkM imeshindwa kusaidia jamii jinsi ya kuwa na viongozi bora na matokeo yake ni kwa viongozi kuichukia jamii ambayo SkM imefanyika (Materego 2002: 144-145; Shule 2010: 153).

Labda tujiulize matokeo ya tafiti hizi hupelekwa kwa nani. Kimsingi na kiutendaji, matokeo haya hurudishwa kwa yule aliyetoa pesa za kuwezesha utafiti kufanyika na mara chache sana jamii husika inaweza kupata taarifa (Samba 2005: 74; Shule 2010: 169). Waandishi Wallace, Bornstein, & Chapman (2007: 40) wanadai kuwa kwa kuwa SkM nyingi zimekuwa zikifadhiliwa zaidi na wafadhili toka nje kupitia asasi zisizo za kiserikali (NGOs), ni wazi kuwa matokeo ya tafiti hizi ndiyo yanayoipa nguvu mifumo ya ubeberu, ubepari na uliberari namna ya kuweza kuendelea kupenyeza ‘mirija’ yake. Na kwa kuwa mifumo hii imejikita katika kusheheneza matabaka kama njia mojawapo ya kuendelea kuitawala dunia, mifumo ya asasi nyingi zisizo za kiserikali inajikuta katika ‘mtego’ wa kuendeleza ubeberu. Jim Igoe na Tim Kelsall (2005: 2) wanasema kuwa dhana ya kuwepo kwa asasi zisizo za kiserikali ni ya kuendekeza mradi wa uliberali, kitu kinachowachora wenye taasisi hizo kama wamisionari wa ukoloni mamboleo – wakala wa ubeberu wa kitamaduni.

Ni wazi kuwa utaratibu wa SkM kumilikiwa na wafadhili unasababisha dhana ya uvamizi wa kiutamaduni (*cultural invasion*) kama Freire (2011: 49) alivyotahadharisha. Watafiti na waraghibishi wengi wanalazimika kutumia njia mbalimbali kwa ajili ya kuweka kumbukumbu. Njia hizi ni kamera za picha za mnato na video pamoja na vinasa sauti. Utaratibu huu unapoangaliwa kwa undani haulengi kumpatia mwanajamii husika kumbukumbu hizo, bali mwenye pesa (mfadhili) ili kuthibitisha matumizi ya hela zake. Huu ni utaratibu wa kuwatumia wanajamii kama mashahidi wa matumizi ya pesa, ambazo kwa asilimia kubwa hurudi mifukoni mwa wafadhili na watafiti (Schininà 2004: 27; Wallace, Bornstein & Chapman 2007: 39-41). Huu ni udhalilishaji unaolenga kuwathibitishia wafadhili kuwa kazi imefanyika au inaweza kufanyika kwa uzuri zaidi iwapo watatoa pesa katika msimu wa fedha unaofuata.

Gibbs (1999: 125-126) ameonesha wazi kuwa kadri muda unavyokwenda, lengo na manufaa ya SkM yanahama kutoka kwa walengwa ambao ni wanajamii kwenda kwa watu binafsi. Hii inatokana na ukweli kuwa matatizo binafsi, mfumo wa uchumi na hasa sera za Benki ya Dunia zimesababisha wanaharakati na wasanii wengi wa Kiafrika kutafuta fedha kutoka kwa wafadhili.

Na ni dhahiri kuwa mataifa mengi ya Kiafrika yako katika lindi la madeni na hata dola zimeshindwa kusaidia sanaa na miradi ya maendeleo ya wananchi wao. Jenerali Ulimwengu (2007) anaangalia dola inayotegemea ufadhili kama dola ya vikaragosi na mateka. Kwani si rahisi kwa dola inayotegemea ufadhili kuweza kujiamulia mambo yake yenyewe.

Lengo la SkM, kama ilivyo kwa sanaa nyingine, siyo kutekeleza maendeleo bali ni kutoa habari zinazohusu maendeleo na kuamsha ari ya kusaka maendeleo kwa wanajamii. Ikiwa maonesho ya SkM yatatumika kama njia ya kupima maendeleo, ni lazima kuwe na uangalifu na uadilifu wa hali ya juu. Hii inatokana na ukweli kuwa maendeleo yoyote lazima yapimwe kwa vigezo mbalimbali. Upimaji wa maendeleo kwa 'tarakimu na herufi' ndio changamoto kubwa ya dhana nzima ya maendeleo. Mfano, ikiwa maendeleo ni maji safi, basi ni lazima kujua watu wangapi wameyapata na hao wasiopata ni asilimia ngapi. Hivyo iwapo maonesho ya SkM hayatatumiwa kwa uangalifu na uadilifu yanaweza kupotosha takwimu. Iwapo lengo ni kujua watu wangapi wameona onesho, wangapi wameuliza maswali na wangapi ni wake na wangapi ni wanaume, ni rahisi kupata namba za kuridhisha.

## Hitimisho

Makala hii imejikita kuangalia kiundani historia ya Sanaa kwa Maendeleo (SkM), matumizi yake na zaidi undumilakuwili wake. Katika historia, tumeona wazi kuwa harakati za SkM nchini Tanzania zilianzishwa na wanazuoni wa Idara ya Sanaa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Lengo likiwa kuwapa wanajamii fursa ya kutumia sanaa zao zilizokuwepo kabla ya ukoloni kama njia ya kuona, kuchambua na kutafuta ufumbuzi wa matatizo yao. Tumeona pia kuwa pamoja na uwezo wa SkM kufanya jamii ijiweze, kwa upande mwingine jamii imewezwa. Ufadhili wenye mrengo wa uliberali mamboleo ni moja ya changamoto za wa utekelezaji wa SkM.

Nina imani kuwa tafiti zaidi kuhusu Sanaa kwa Maendeleo ya kiliberali mamboleo ni muhimu. Ila ni lazima tafiti hizi zilenge kupambanua mifumo ya kisiasa na kiuchumi ya dunia ambayo mara nyingi imekuwa 'mizigo' kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania. Siyo sahihi kuamini kuwa SkM ya miaka ya 1980 inaweza kufanyika katika mazingira na utaratibu ule ule wakati ilipobuniwa. Pia ni vizuri kuangalia dhana ya uvamizi wa kitamaduni inavyosanifishwa na SkM badala ya dhana halisi ya umiliki wa SkM. Na ni jambo la muhimu kuhoji sanaa hii inayoitwa Sanaa kwa Maendeleo, ni kwa maendeleo ya nani – mwanajamii, mtafiti au mfadhili?

Kwa kuangalia kijuujuu tu, lengo la SkM ni kumletea mwanajamii maendeleo ili ajiweze. Ila kwa undani ni kumnyang'anya nguvu inayomwezesha kupata maendeleo yake mwenyewe, yaani mwanajamii amewezwa. Kwa mtazamo wangu, ingawa mfumo wa 'utandawazi' (ubeberu) unalazimisha kuwa 'usipoweza kupambana nao, basi jiunge nao', sanaa hata kama imeshindwa kupambana na uliberali mamboleo bado ina nafasi ya kutojiunga nao. Ninaamini sanaa iliyojikita katika

kutumia fasihi na kuboresha umbuji inaweza kupambana na mifumo inayotaka kuimeza na kuifanya sehemu ya maslahi 'yao'. Na mwisho, kuhusu uhusiano wa SkM na ufadhili, hoja ya msingi inabaki pale pale, "wanja wa manga si dawa ya chongo."

**Marejeleo**

Askew, Kelly. 2002. Performing the Nation: *Swahili Music and Cultural Politics in Tanzania*. Chicago: University of Chicago Press.

Bakari, Juma A., & Materego, Gonche R. 2008. *Sanaa kwa Maendeleo: Stadi, Mbinu na Mazoezi*. Moshi: Viva Productions.

Boal, Augusto. 2000. *The Theatre of the Oppressed.* London: Pluto Press.

Carlson, Marvin. 2001. *The Haunted Stage*. Ann Arbor: Michigan Press.

Chachage, Chambi S. & Chachage, Seithy L. 2004. Nyerere: Nationalism and Post-Colonial Developmentalism. *African Sociological Review 8, 2*: 158-179.

Diagne, Souleymane Bachir, & Henri Ossébi 1996. The Cultural Question in Africa: Issues, Politics and Research Prospects. *Working Paper/CODESRIA* No.3.

Epskamp, Kees. 2006. *Theatre for Development: An Introduction to Context, Applications and Training.* London & New York: Zed Books.

Etherton, Michael. 2004. South Asia's Child Rights Theatre for Development: The Empowerment of Children who are Marginalized, Disadvantaged and Excluded. *Theatre and Empowerment: Community Drama on the World Stage*, ed. By Richard Boon, & Jane Plastow. Cambridge: Cambridge University Press. pp.188-218.

Eyoh, Hansel Ndumbe. 1984. *Hammocks to Bridges: An Experience in Theatre for Development.* Yaoundé: BET.

Fosu, Augustin Kwasi. 2008. Anti-growth Syndromes in Africa: A Synthesis of the Case Studies. *Political Economy of Economic Growth in Africa 1960-2000*, ed. by Benno J. Ndulu, Stephan A. O'connell, Robert H. Bates, Paul Collier & Chukwuma C. Soludo, Cambridge: Cambridge University Press. pp. 137-172.

Freire, Paulo. 2011. *Cultural Freedom in Latin America*. Educacion Global Research: http://educacionglobalresearch.net/wp-content/uploads/01-Freire-English.pdf (ilisomwa mara ya mwisho 15-03-2013).

Gibbs, James. 1999. Noticeboard. *African Theatre in Development*, ed. by Martin Banham, James Gibbs & Femi Osofisan. Oxford: James Currey. pp 125-126.

Igoe, Jim, & Kelsall, Tim (Eds.). 2005. *Between a Rock and Hard Place: African NGOs, Donors and the State.* Durham: Carolina Academic Press.

Kerr, David.1995. *African Popular Theatre: From Pre-Colonial Times to the Present Day.* London: James Currey.

Lange, Siri. 2002. *Managing Modernity: Gender, State, and Nation in the Popular Drama of Dar es Salaam.* PhD, University of Bergen.

Lihamba, Amandina. 1985. *Politics and Theatre After the Arusha Declaration, 1967-1984.* PhD, University of Leeds.

Lihamba, Amandina 2004. Tanzania. *A History of Theatre in Africa*, ed. by Martin Banham. Cambridge: Cambridge University Press. pp. 233-246.

Lihamba, Amandina. 2007. *Gender Perspective in Arts and Cultural Education.* Bagamoyo: The Norad Programme in Arts and Cultural Education (ACE).

Materego, Gonche R. 2002. *Popular Theatre in Question: The Issue of Sustainability.* MA, University of Dar es Salaam.

Mlama, Penina M..1991. *Culture and Development: The Popular Theatre Approach to Africa.* Uppsala: Scandnavian Institute of African Studies.

Mlama, Penina M. 2005. *Empowering Girls Out of the Gender Trap: The TUSEME Experience in Africa.* Uppsala: Nordic Institute.

Ndagala, Daniel K. 2007. *Utamaduni na Dhima Yake katika Maendeleo.* Dar es Salaam: Tanzania Culture Trust Fund.

Ngũgĩ wa Thiong'o. 2013. *Wasomi, Lugha za Ulaya na za Afrika: Kati ya Kujiweza na Kuwezwa. Dar es Salaam, Tanzania*. Mhadhara uliotolewa katika ukumbi wa Nkrumah, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Novemba, 22, 2013.

Nyerere, Julius. 1968. *Freedom and Socialism.* Dar es Salaam: Oxford University Press.

Nyoni, Frowin Paul. 2008. Sanaa kwa Maendeleo na Athari za Ufadhili, Tanzania. *Wasanii na Sanaa za Maonesho Mashariki mwa Afrika: Changamoto Katika Karne ya 21*. Dar es Salaam: Eastern Africa Theatre Institute. pp. 169-176.

Odhiambo, Christopher J. 2008. *Theatre for Development in Kenya: In Search of an Effective Procedure and Methodology*. Bayreuth: Bayreuth African Studies.

Plastow, Jane. 2009. Theatre for Development: A Business Opportunity, a Tool of Oppression, or a Road to Empowerment? *African Theatre Association-New Directions in African Theatre and Performance*. Northampton: AfTA Book of Abstract. pp.17.

Samba, Emelda N. 2005. *Women in Theatre for Development in Cameroon: Participation, Contributions and Limitations.* Bayreuth: Bayreuth African Studies.

Schininà, Guglielmo. 2004. Here Were Are; Social Theatre and Some Open Questions About its Developments. *The Drama Review 48: 3 (T183)*: 17-31.

Sen, Amartya. 2000. *Culture and Development.* World Bank Tokyo Meeting 13-12-2000. http://info.worldbank.org/etools/docs/voddocs/354/688/sen_tokyo.pdf (ilisomwa mara ya mwisho tarehe 28-02-2015).

Shivji, Issa G. 2007. The Story of Independence: From Nationalism to Neo-liberalism. *Sunday Palaver*. Sunday News 2007.

Shivji, Issa G. 2009. *Accumulation in an African Periphery: A Theoretical Framework.* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Shule, Vicensia. 2010. *Beyond Socialism: Tanzanian Theatre, Neoliberalism and Foreign Aid Complexity*. Mainz: PhD, Johannes Gutenberg-University Mainz.

Shule, Vicensia. 2011. Theatre in/for Development in Africa: Neoliberal Nightmare. *Trends in Twenty-first Century African Theatre and Performance*, ed. by Kene Igweonu. Amsterdam: RODOPI. pp.190-215.

Ulimwengu, Jenerali. 2007. Ili Tuendelee, Hatuhitaji Vitu Vingi. *Raia Mwema*. 31-10-2007. http://www.raiamwema.co.tz/ili-tuendelee-hatuhitaji-vitu-vingi (ilisomwa mara ya mwisho tarehe 01-03-2015)

Wallace, Tina; Bornstein, Lisa & Chapman, Jennifer. 2007. *The Aid Chain: Coercion and Commitment in Development NGOs.* Schottsville: University of Kwa Zulu-Natal Press.

Ziegler, Lauren. 2009. *Tuseme: Girls' Empowerment Theatre for Development Clubs.* Changemakers. 10-06-2009. http://www.changemakers.com/en-us/node/52364 (ilisomwa mara ya mwisho tarehe 05-01-2010).